

4 ZANZIBAR LEO Jumatatu 4 Juni, 2018 MAONI / UCHAMBUZI / KATUNI

MAONI YETU

TUUTUMIE MRADI WA KUSARIFU TAKA KUPUNGUZA UCHAFUZI MAZINGIRA

ZANZIBAR inazalisha zaidi ya tani 280 za taka kwa siku, huku asilimia 50 tu ya taka hizo ndizo zinazotupwa katika jaa kuu liliopo Kibele.

Takwimu hizi zinamaanisha kwamba zaidi ya tani 8,400 za taka zinazalishwa kwa mwezi lakini ni tani 4,200 tu ndio zinazotupwa na kiwango kilichosalla kikibalia mitaani na kuwa chanzo cha uchafu.

Kiwango kikubwa cha taka hizo zinazalishwa katika Mji Mkongwe wa Zanzibar ambao una idadi kubwa ya hoteli za kitalii na ndio mji unaotembelewa na watalii wengi.

Lakini cha kusikitisha, baadhi ya mitaa ya mji huu, majaa makubwa ya kutupia taka yapo mbele ya hoteli za kitalii.

Kwa muda mrefu, Baraza la Manispaa Mjini, linalalamikia changamoto mbali mbali zinazosababisha taka kushindwa kuzolewa kwa wakati.

Changamoto hizi ni pamoja na upungufu wa gari za kusombea taka, wafanyakazi, gharama za uendeshaji wa gari za kubebea taka pamoja na umbali wa eneo lilipo jaa la kutupia taka.

Changamoto nyengine ni wananchi wenyewe kushindwa kuvitumia vifaa vilivyowekwa kwa ajili ya kuhifadhi taka hali inayosababisha taka kuzagaa mitaani.

Hata hivyo, katika kipindi cha hivi karibuni kuna juhudi zinazochukuliwa kuzitumia taka kama rasilimali kwenye shughuli za maendeleo.

Tayari mradi wa kuzigeuza taka kuwa rasilimali badala ya nakama umeanzishwa katika mtaa wa Shaurimoyo, ukisimamiwa na kituo cha sayansi na mazingira cha India (CS).

Kituo hiki kitazisarifu taka zinazozalishwa maeneo mbali mbali na kutumika kwenye shughuli nyengine ikiwemo uzalishaji wa mbolea itakayotumika kwenye kilimo.

Mradi huu tunaamini unaweza kuwa mkombozi kwa wananchi na pia utapunguza changamoto kubwa kwa manispaa.

Hata hivyo, taka zitakazotumiwa kwenye mradi huu ni zile kavu hivyo basi bado kutakuwa na tatizo la taka zinazooza, ambazo ndio zinazozalishwa kwa wingi.

Kwa kuwa mradi huu ndio kwanza unaanza, ni nafasi sasa kwa manispaa kutoa elimu kwa wananchi juu ya uhifadhi mzuri wa taka.

Aidha iweke vifaa maalum kwa ajili ya utupaji wa taka kavu na jengine kuhifadhi taka zinazooza.

Tukifanya hivyo, tutasaidia mradi huu kufanikiwa lakini pia kupunguza tatizo la taka nchini na hivyo kuuweka mji wetu katika mandhari ya kuvutia.

LEO JUMATATU JUNI 4, 2018
SAWA NA MWEZI 19 RAMADHANI 1439
MWAKA WA KIISLAMU



NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Abdalla Hassan Mitawi, kifungua mkutano wa wadau wa mazingira uliofanyika hoteli ya Marumaru Forodhani mjini Unguja. (PICHA NA ALI HAMAD, ZEMA).